
Ocular films

TUMIA AI KWENYE CONTENT BILA KUDANGANYA WATEJA



AI ikufanyie nini kwenye content ya biashara yako, isikufanyie nini, na jinsi ya kujua tofauti kabla hujapost.

FREE GUIDE NA
Med · @he.is.med

IMELETWA NA
Ocular Films

KWA AJILI YA
Wafanyabiashara wote

Kanuni moja kuu

Tumia AI kufanya content yako iwe nzuri na ya haraka. Usiitumie kutengeneza proof.

01

Msaada

AI ikusaidie kazi nzito: ideas, scripts, captions na editing.

02

Proof


Matokeo, reviews na before & after lazima ziwe za wateja halisi.

03

Uwazi

Kama mtu anaweza kudhani ni kitu halisi, mwambie ni AI.

Taa tatu za AI



Kabla hujatumia AI kwenye post, jiulize iko kwenye taa gani. Kijani ni ruksa, njano weka label, nyekundu hapana kabisa.

KIJANI	NJANO	NYEKUNDU
Tumia bila wasiwasi	Tumia, ila weka label	Usi-fake kamwe
Ideas na scripts	**Picha na scenes za AI**	**Before & after**
Captions na replies	**Sauti na avatars za AI**	**Reviews za wateja**
Editing na subtitles	**Edits nzito za picha**	**Bidhaa inachofanya**

Mteja atakusamehe kwa kutumia AI. Hatakusamehe ukimdanganya kwa kutumia AI.

Kijani: AI ikufanyie kazi nzito

Hapa AI inakuokolea masaa mengi, na hakuna anayedanganywa.



Ideas na scripts

AI ni partner mzuri wa ku-brainstorm. Chukua ideas zake kama draft, halafu weka stori zako halisi.

JARIBU HII

"Nipe ideas 10 za video zinazojibu maswali ya wateja wangu kabla hawajanunua ___."

Captions na replies

Andika captions, majibu ya FAQ na replies za DM haraka. Ila soma kwanza kabla ya kupost.

JARIBU HII

Weka swali la mteja, iombe ikupe jibu fupi na la kirafiki kwa style yako.

Editing na subtitles

Auto-subtitles, kusafisha sauti na kukata sehemu za kimya. Footage ni halisi, imenyooshwa tu.

JARIBU HII

Pitisha video yako ijayo kwenye auto-captions, halafu rekebisha maneno yaliyokosewa.

Njano: tumia, ila weka label



Ni sawa kutumia, ilimradi mtu asidhani ni picha halisi, mtu halisi au tukio halisi.

Picha na scenes za AI

Nzuri kwa concepts, backgrounds na mood. Sio kwa kuonyesha bidhaa yako inavyoonekana.

WEKA LABEL HIVI

"Picha hii imetengenezwa kwa AI" kwenye caption au screen.

Sauti na avatars za AI

Tumia sauti yako mwenyewe au yenye license. Kamwe usitumie ya mtu mwingine bila ruhusa yake.

WEKA LABEL HIVI

"Voiceover imetengenezwa kwa AI" mwisho wa caption.

Edits nzito za picha

Retouch kidogo ni kawaida. Kubadilisha rangi, size au quality ya bidhaa sio.

WEKA LABEL HIVI

Weka na picha moja ya bidhaa halisi, bila edit, kwenye post hiyo hiyo.

Nyekundu: usi-fake hivi kamwe

Hii ndio proof. Ikishakuwa fake, sio proof tena, ni uongo.



Before & after

Matokeo ya AI yanaahidi kitu ambacho bidhaa yako haiwezi kufanya. Mteja atagundua siku ya delivery.

FANYA HIVI BADALA YAKE

Rekodi wateja halisi kwa ruhusa yao, hata kama mabadiliko ni madogo.

Reviews za wateja

Sura na sauti za AI zinazojifanya wateja walioridhika zinaua trust milele.

FANYA HIVI BADALA YAKE

Waombe wateja 3 halisi video ya sekunde 10 au screenshot ya WhatsApp.


Bidhaa inachofanya

Kama post inaonyesha kitu ambacho bidhaa haifanyi, huo ni utapeli wa matangazo.

FANYA HIVI BADALA YAKE

Onyesha bidhaa halisi ikitumika, kwenye mwanga halisi, na mtu halisi.

Maswali 6 ya kujiuliza kabla ya kupost



Pitisha kila post uliyotumia AI kwenye maswali haya. Jibu moja likiwa baya, rekebisha kwanza.

1	Mteja wangu atajisikia kudanganywa akijua hii imetengenezwa vipi?
2	Hii ni matokeo, review au bidhaa yenyewe? Basi lazima iwe halisi.
3	Kila mtu halisi aliyeonekana ametoa ruhusa ya sura na sauti yake?
4	Nimeweka label kwenye kila kitu kinachoonekana halisi ila ni AI?
5	Nimecheki facts, bei na spelling ambazo AI imeniandikia?
6	Bado inasikika kama sisi, sio kama robot?

Mambo ya kufanya, na mambo ya kuepuka

Fanya	Epuka
Tumia AI kwa ideas, halafu weka stori zako halisi	Video fake za before & after
Rekodi wateja halisi na bidhaa halisi	"Wateja" wa AI wakitoa reviews
Weka label kwenye picha na sauti za AI zinazoonekana halisi	Filters zinazobadilisha muonekano wa bidhaa
Cheki kila fact na bei ambayo AI imeandika	Kupost maandishi ya AI bila kuyasoma
Sura na sauti yako ibaki kwenye content	Kutumia sura au sauti ya mtu bila ruhusa yake

Mfahamu creator



Med

@he.is.med

Filmmaker, content creator & strategist
Certified Public Accountant (CPA) · AI Native

Now nimefanikisha ukuaji wa brands mbalimbali kupitia content, zikiwemo brands zangu mwenyewe. Kila kilichopo kwenye hii pdf ni vitu ninavyovifanyia kazi kila siku kwa wateja wangu na kwenye biashara zangu binafsi.

Hii guide ya bure ni favor yangu kwako. Sasa nitafurahi kama na wewe utanifanyia favor kwa ku-follow business pages zangu.

Ocular Films

Creative production company: commercials, UGC na social media content kwa biashara.

@ocular.films
ocularfilms.com

TimePoint Dar

Saa original kwa bei unayoiweza, tunakuletea popote Dar es Salaam.

@timepointdar
timepointdar.com

Lux Wedding Experience

Wedding films na picha zinazokufanya uikumbuke siku yako tena na tena.

@luxweddingexperience
luxweddingexperience.com

Unahitaji content ya biashara yako? DM @ocular.films au tembelea ocularfilms.com